# Asili ya METHODISTI

GLOBAL METHODIST CHURCH

**Askofu Scott Jones** – Umethodisti katika ubora wake unalingana kikamilifu na Ukristo halisi. Kama John Wesley alivyosema, ni dini ya Biblia, dini ya kanisa la awali na dini ya Kanisa la Uingereza. Sisi kama Wamethodisti Ulimwenguni tunataka kukumbatia yaliyo bora zaidi ambayo ni urithi na utamaduni wetu. Lakini hiyo inamaanisha tunahitaji kuukumbuka na kuuelewa.

**Askofu Leah Gregory** – Kanisa letu lilianza kama vuguvugu kwenye Kanisa la Uingereza katika miaka ya 1700. Wakati huo, sehemu nyingi za kanisa lililoanzishwa zilikuwa na kiwango cha chini cha kiroho. Watu walikuwa wakihama kutoka mashambani kwenda mijini kadiri Enzi ya Mageuzi ya Viwanda ilivyoendelea. Ukristo ulikuwa umekuwepo nchini Uingereza kwa karne nyingi na ulikuwa dini rasmi ya nchi nzima. Kulikuwa na madhehebu mengine ya Kiprotestanti yaliyoruhusiwa kuendelea, lakini kila mtu alichukuliwa kuwa mshiriki wa Kanisa la Uingereza isipokuwa kama alishiriki kikamilifu katika mojawapo ya makanisa hayo mengine. Jumuiya kadhaa za kidini zilianzishwa wakati huu, huku zikinuia kupinga baadhi ya mitindo hii.

**Askofu Kimba Evariste** – John Wesley aliuliza swali, "Tunaweza kuamini kwa busara kuwa mpango wa Mungu ni upi katika kuwakuza wahubiri wanaoitwa 'Wamethodisti'?" Jibu lake, ambalo liliwekwa katika "Kumbukumbu Kubwa" … hati ambayo baadaye ilikuwa Kitabu cha Mafundisho na Nidhamu … lilikuwa hivi: "Kurekebisha taifa, na hasa Kanisa, kueneza utakatifu wa kimaandiko katika nchi yote." Umethodisti ulikuwa vuguvugu lenye nia ya kubadilisha Kanisa na taifa lote.

**Askofu Eduard Khegay** – Lilianza kama jamii katika Kanisa, likiwa na nia ya kuboresha ushuhuda wake. Katika miaka ya 1700 hakukuwa na tofauti za kimafundisho kati ya jamii za Kimethodisti na Kanisa. Ujumbe waliohubiri ulikuwa sawa na mafundisho rasmi ya Kanisa la Uingereza. Hata hivyo, wahubiri walilenga kuinua msimamo wa kiroho na desturi za watu kwa kuwakumbusha kile ambacho kanisa liliamini rasmi. Huu ulikuwa mwito wa uamsho.

**Askofu Mark Webb** – Walei wa Kimethodisti walihamia Amerika na vuguvugu hilo likaanzishwa huko. Wahubiri walitumwa kuongoza vuguvugu hilo na likakua. Marekani ilipopata uhuru, John aliamua kwamba ulikuwa wakati wao kuwa kanisa huru. Alimteua Thomas Coke kuwa mrakibu, na baadaye Coke akamweka Francis Asbury wakfu. Muda mfupi baadaye, wawili hao waliitwa maaskofu.

Hadithi ya Umethodisti imefungamana na safari za kiroho za ndugu wa Wesley. John na Charles walilelewa katika nyumba ya mchungaji mjini Epworth. Baba yao Samuel alichapisha vitabu kadhaa vya kitaaluma lakini hakuthaminiwa sana kama mchungaji. Mama yao aliyeitwa Susannah alikuwa mwanamke aliyesoma na aliendeleza huduma yake katika parokia. Samuel alipokuwa safarini kwa muda mrefu, Susannah aliongoza sala za jioni nyumbani mwao, zilizohudhuriwa na watu wengi sana. Samuel alipomwambia aache (kwa sababu wanawake hawakupaswa kufundisha kanisani), alikataa na kusema kwamba angeacha tu ikiwa angempa amri dhahiri ya kufanya hivyo. Aliendelea.

Mnamo 1709, nyumba ya Wesley (yaani nyumba ya paroko) ilichomwa. John alikuwa bado katika chumba cha juu nyumba ilipokuwa ikiteketea, na majirani walilazimika kunyosha mikono juu na kumvuta kupitia dirishani. John aliamini daima kwamba maongozi ya Mungu ndiyo yaliyomwokoa, kulingana na Zekaria 3:2: "kijinga kinachowaka kilichonyakuliwa kwenye moto."

**Askofu Eduard Khegay** – Hatua ya kwanza ya kuibuka kwa Umethodisti ilikuwa kuanzishwa kwa kikundi cha wanafunzi katika Oxford. Kwa kuwa John alikuwa Fellow (mshirika wa kitaaluma) wa Chuo cha Lincoln, alichukua uongozi wa kikundi hicho ingawa Charles ndiye aliyekianzisha. Walihimizana kuhudhuria ibada kila wiki na walikutana pamoja kwa ajili ya maombi na mafunzo. Walianza kuwatembelea wafungwa na kuwasaidia wanafunzi maskini ili wapate elimu. Baada ya muda, wengine waliita kikundi hiki "Wanasakramenti," "Nondo wa Biblia," "Klabu Takatifu," na hatimaye "Wamethodisti." Jina hilo la mwisho ndilo lililodumu, na mara kwa mara John alitumia usemi "watu wanaoitwa Wamethodisti."

**Askofu Scott Jones** – Hatua ya pili ya kuibuka kwa Umethodisti ilianza wakati John na Charles, pamoja na marafiki zao wawili, walipokwenda kuhudumu katika koloni la Georgia nchini Amerika. Tukio muhimu kwa vuguvugu la Kimethodisti lilikuwa ni kukutana kwa John Wesley na Wamoravia kwenye meli iliyokuwa ikienda Georgia. Wakati wa dhoruba aliogopa kufa kwa sababu hakuwa na hakika ya wokovu wake. Wamoravia waliimba nyimbo wakati wa dhoruba na walikuwa imara katika imani yao. Wesley alifanya mazungumzo muhimu na Wamoravia katika koloni ya Georgia na pia baada ya kurudi Uingereza. Mnamo 1738 walianzisha Fetter Lane Society na walimfundisha kuhusu mikutano ya bendi na kumsaidia kukumbuka mafundisho rasmi ya Kanisa la Uingereza. Mnamo Mei 21, 1738 Charles alipata ugeuzaji ambao umeelezewa katika wimbo wake wenye nguvu "And Can It Be". Siku tatu baadaye, John alikuwa katika kikundi kidogo ndani ya nyumba iliyokuwa Aldersgate Street, ambako mtu fulani alikuwa akisoma Dibaji ya Martin Luther ya Kitabu cha Warumi. Alielezea jambo alilopitia usiku huo kwa maneno haya: "Karibu na saa tatu kasorobo, alipokuwa akielezea mabadiliko ambayo Mungu hufanya moyoni kupitia imani katika Kristo, nilihisi moyo wangu ukipata joto kwa namna ya ajabu. Nilihisi kwamba nilimtegemea Kristo, na Kristo pekee kwa ajili ya wokovu, nami nikapewa hakikisho kwamba alikuwa ameziondoa dhambi zangu, naam, zangu mwenyewe, na kuniokoa mimi kutoka katika sheria ya dhambi na mauti." Ingawa baadaye John alipitia matukio ya kupanda na kushuka kiroho, tukio la Aldersgate Street lilikuwa hatua muhimu ya mabadiliko katika huduma yake.

**Askofu Leah Gregory** – Kuna vipengele vitano vikuu vya vuguvugu la mapema la Kimethodisti ambavyo tunastahili kuzingatia sasa. Kwanza, walirudisha mwelekeo wa utakatifu wa kimaandiko. Theolojia ya John iliundwa kwanza kwa kujitolea kwake kwa dhati kuishi maisha matakatifu, kulikotokana na ushawishi wa wazazi wake tangu utotoni. Alifuata amri za Mungu kwa makini tangu utotoni. Kisha mnamo 1725 alisoma kitabu cha Uigaji wa Kristo cha Thomas à Kempis na cha Sheria na Mazoezi ya Kuishi na Kufa Kitakatifu cha Askofu Jeremy Taylor. Hii ilimwongezea hamu ya kutafuta utakatifu upande wake. Alianza kuweka shajara ili kupima jinsi alivyokuwa akitumia muda wake vizuri katika harakati za kutafuta utakatifu. Pamoja na washiriki wengine wa Klabu Takatifu huko Oxford alishiriki katika matendo mengi mema kama vile kutembelea wafungwa na kuanzisha shule ya watoto maskini. Hata hivyo, Wesley hakuwa na hakika kwamba alikuwa mtakatifu vya kutosha, na alipokutana na Wamoravia alianza kutilia shaka wokovu wake mwenyewe. Katika miaka muhimu ya 1735–1738, alifikia uelewa kwamba utakaso kamili kwa hakika ulikuwa mapenzi ya Mungu kwa kila mtu, na kwamba unatimizwa tu kwa neema kupitia imani katika Kristo.

**Askofu Mark Webb** – Kifungu cha Waefeso 2:8–10 kikawa mojawapo ya vifungu alivyovipenda sana. "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kupitia imani, nayo

haikutokana na ninyi wenyewe. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, si kwa matendo, ili mtu yeyote asije akajisifu. Kwa maana sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili tupate kutenda matendo mema, ambayo Mungu alitangulia kuyaandaa tupate kuishi katika hayo." Utakatifu unamaanisha kutimiza amri za Mungu: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote" na "Mpende jirani yako kama nafsi yako." (Mathayo 22:37, 39)

Wamethodisti wana historia ndefu ya kutafuta utakatifu. Uelewa wetu wa Maandiko unasema kwamba utakatifu huo ni kipawa cha Mungu. Tunapotumia neno utakatifu wa kimaandiko tunasema kwamba ni neema ya Mungu inayotubadilisha kupitia imani. Mungu aliahidi haya kupitia Ezekieli akisema, "Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama." (Ezekieli 36:26). Mungu anatenda kupitia Roho Mtakatifu kutupa tunda linaloelezwa katika Wagalatia 5:22–23: upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi. Mapenzi ya Mungu kwetu ni utakaso wetu, na Mungu anafanya kazi kwa hima katika maisha ya wafuasi wake ili kuendeleza utakatifu wetu.

**Askofu Kimba Evariste** – Kipengele cha pili ni kwamba Wamethodisti walieneza injili mahali watu walipokuwa. Rafiki wa akina Wesley kutoka Oxford, George Whitefield naye alikuwa amepata ugeuzaji na alikuwa akihubiri wokovu kwa njia ya imani. Kama wao, aliambiwa kwamba hangekaribishwa tena katika maeneo mengi. Whitefield alianza kuhubiri nyanjani na akagundua kwamba umati mkubwa ulikuja kumsikiliza. Alimwalika John aende Bristol na kuhubiri huko pia. Kuhubiri nje ya kanisa ilikuwa tabia isiyo ya kawaida kwa wakleri wa Kanisa la Uingereza. Ingawa haikuwa kinyume cha sheria moja kwa moja, haikukubalika kabisa kwa sababu iliwakumbusha watu machafuko ya karne iliyotangulia.

Hata hivyo, mnamo Aprili 2, 1739, John aliandika kwamba "alikubali kuwa duni zaidi" na akahubiri katika uwanja kwa "watu elfu tatu au nne." Hii ilikuwa mara ya kwanza kwake kujihusisha na kuhubiri nyanjani, jambo ambalo lilikuwa desturi ya vuguvugu la Kimethodisti. Hata Wamethodisti walipokuwa na nyumba za mahubiri walizokuwa wakisimamia, John aliwahimiza kuhubiri nyanjani ili kuwafikia watu.

**Askofu Scott Jones** – Kipengele cha tatu cha Umethodisti wa awali kilikuwa matumizi ya Wesley ya walei kuhubiri na kueneza injili. Wesley aligundua siku moja kwamba mmoja wa wasaidizi wake—mtu wa kawaida aliyeitwa Thomas Maxfield—alikuwa ameanza kuhubiri wakati alikuwa nje ya mji. Vuguvugu hilo lilikuwa linawafikia watu wengi na walikuwa wakiunda jamii nyingi mpya. Ndugu wa Wesley hawakuweza kuwa kila mahali! Hapo mwanzo, Wesley alifikiri kwamba watu wa kawaida hawapaswi kuruhusiwa kuhubiri. Lakini mama yake alimwonya kuhusu Maxfield akisema "Jihadhari na kile unachofanya kuhusiana na kijana yule, maana ameitwa hakika na Mungu kuhubiri jinsi wewe ulivyo. Chunguza matunda ya mahubiri yake na umsikilize wewe mwenyewe pia." Kuanzia wakati huo Wesley alianza kuruhusu watu wa kawaida kuhubiri. Aliwakusanya katika makongamano ya kila mwaka yaliyolenga maswali matatu: Nini cha kufundisha? Ni namna gani ya kufundisha? Na nini cha kufanya? Pamoja na wasaidizi hawa walei, Umethodisti ulianzisha jamii mpya kote Uingereza, Uskoti, Ayalandi na Wales. Tangu wakati huo, Wamethodisti wamekuwa wakiwahusisha walei katika huduma na kufanya makongamano ya kila mwaka.

**Askofu Mark Webb** – Nne, Wamethodisti wa awali walianzisha vikundi vidogo vya uwajibikaji. Mnamo 1738, Wesley alikuwa akifanya kazi na jumuiya kadhaa za kidini huko Bristol na akagundua kwamba huduma yao ingekuwa imara zaidi kama wangekuwa na mahali maalumu pa kukutania. Alichukua mkopo na kujenga nyumba ya kuhubiria iliyoitwa Chumba Kipya. Lakini ujenzi huo ulisababisha deni, na Wesley alihitaji njia ya kulilipa. Watu waliamua kwamba kila mtu angetoa senti moja kwa wiki na kwamba wangegawanywa katika vikundi vya watu kumi na wawili ili kukusanya fedha hizo. Muda mfupi baadaye, watu hawa walianza kukutana, na kiongozi akaanza kumuuliza kila mmoja, "Nafsi yako iko vipi?" Huu ulikuwa mwanzo wa mikutano ya wengi.

Wesley alijitolea kuishi maisha matakatifu na aliona mikutano ya wengi kuwa desturi muhimu iliyowasaidia watu kukaribia utakatifu. Muda mfupi baadaye, kuhudhuria mikutano ya wengi kukawa sharti la kuwa mshiriki wa jamii ya Kimethodisti. Alipotembelea jamii ya Kimethodisti huko Newcastle mnamo 1743, aligundua watu ambao hawakuwa wakifuata utakatifu. Kisha akatayarisha "Sheria Jumla za Jamii Zilizoungana." Ikiwa mtu alitafuta wokovu, kulikuwa na sheria tatu.

**Askofu Leah Gregory** – Alisema, "Kuna sharti moja tu linalotakiwa kwa wale wanaotamani kujiunga na jamii hizi: 'hamu ya kuikimbia ghadhabu inayokuja na kuokolewa kutoka katika dhambi zao.' Lakini jambo hili likiwa limekita mizizi moyoni, litaonekana kwa matunda yake. Kwa hiyo, wote wanaoendelea kuwa katika jamii hizi wanatarajiwa kuendelea kuonyesha hamu yao ya wokovu. Kwanza, Kwa kutotenda uovu na kwa kuepuka maovu yoyote—hasa yale yanayotendwa kwa njia ya kawaida zaidi… Pili, Kwa kutenda mema na kuwa na rehema kwa kila namna kadiri ya uwezo wao, wakitumia kila fursa kutenda mema ya kila aina kwa watu wote kadiri inavyowezekana… na Tatu, Kwa kuzingatia maagizo yote ya Mungu."

Sheria hizi za Jumla bado ni sehemu ya mafundisho ya Kanisa la Methodisti Ulimwenguni leo, na tunasisitiza tena kwamba kuwa mshiriki wa kikundi kidogo cha uwajibikaji ni desturi muhimu ya kiroho.

**Askofu Eduard Khegay** – Kipengele cha tano cha vuguvugu la awali la Kimethodisti ni msisitizo wa mbinu za neema kama njia ya kuishi maisha ya Kikristo kwa ujumla. Baadhi ya Wamoravia walikuwa wakiwashauri watu wasipokee sakramenti mpaka wapate uhakika wa wokovu wao. Badala yake, John alisisitiza kwamba Mungu ameweka njia za kawaida ambazo kupitia kwazo huwapa neema watu wanaomtafuta. Mbinu hizi za neema ziliwasilisha neema tangulizi, neema yenye haki na neema inayotakasa, kulingana na hitaji la mtu wakati huo. Ushirika Mtakatifu, kusoma Maandiko, ibada ya hadhara, maombi na kufanya mikutano ya Kikristo—hizo zote zilikuwa njia ambazo Mungu aliweka ili kuwasaidia watu wake katika safari ya wokovu.

**Askofu Kimba Evariste** – Katika "Mawazo Kuhusu Umethodisti," Wesley alieleza hamu yake kwamba vuguvugu alilolianzisha liendelee na "mafundisho yaleyale, roho ileile na nidhamu ileile" lilizoanza nazo. Na iwe hivyo.